

UHURU, Jumatano, Novemba 11, 1987

MAPUTO, Msumbiji: Jumuiya ya Uchumi ya nchi za Ulaya Magharibi (EEC) itatoa msaada wa ulinzi kwa Msumbiji, Ofisa mwandamizi wa umoja huo unaozijumuisha nchi 14 alisema juzi. Naibu Mkurugenzi Mkuu wa EEC anayeshughulikia Maendeleo, Bw. Andre Auclert ambaye aliitembelea Msumbiji alimaliza ziara yake ya siku nane kwa kutiliana saina mkataba ambapo miradi yote inayoendeshwa kwa msaada wa Jumuiya hiyo italindwa dhidi ya mashambulizi yoyote ya hujuma.